

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

BARABAI
S.L.P 484



43108 SINGIDA,
Barua Pepe: rbcasingida@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

SINGIDA – JUNI 29, 2020

TAARIFA KWA UMMA

HAKIMU KIZIMBANI

KWA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA

Leo tarehe 29/06/2020 ofisi ya TAKUKURU mkoa wa Singida inatarajia kuwafikisha kwenye Mahakama ya Wilaya ya Manyoni **Mhe Bahati Manongi Ilikunda** Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kilimatinde na Mzazi mwenzake **Haji Juma Bwegege** ambao kwa pamoja wanatuhumiwa kwa makosa ya kuomba na kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya Mwaka 2007.

Ofisi hii ilipokea Taarifa kutoka kwa mwananchi mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa, kuwa Mhe Bahati Manongi Ilikunda wa Mahakama ya Mwanzo Kilimatinde Wilayani Manyoni anaomba Rushwa ya shilingi 350,000/=, ili atoe upendeleo kwa mtoa taarifa kwenye shauri la madai namba 03/2020, shauri ambalo lipo mbele yake.

Mnamo Tarehe 28/06/2020 huko Wilayani Manyoni mkoani Singida maeneo ya kituo cha mabasi yaendayo Dodoma, Ofisi hii ilimkamata Haji Juma Bwegege ambaye ni mzazi mwenzake na Mhe. Bahati baada ya kupokea rushwa ya shilingi 170,000/= ikiwa ni sehemu ya shilingi 350,000/=zilizoombwa.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Singida umejiridhisha kuwa **Haji Juma Bwegege** na **Mhe Bahati Manongi Ilikunda** wana mahusiano ya kifamilia (Wana mtoto waliyezaa pamoja) jambo linaloashiria uwezekano wa Mhe. Bahati kumtumia Haji katika kupokea rushwa anazoiomba.

Ofisi ya TAKUKURU (M) Singida inatoa shukrani za dhati kwa Idara ya Mahakama mkoani hapa kwa jinsi tunavyoshirikiana kwenye mapambano dhidi ya Rushwa kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama ya Mkoa

Imetolewana:

Signed

Adili Elinipenda

Mkuuwa TAKUKURU (M) Singida
